ajina
aasisi
vasifu
taar-
wake.
a sifa
arifa
Mtan-
watu
ma.
, baa-
waja-
waki-
u vya
doma
nayo-

a nau-
kabila
utu-
mishi
za na

kwe-
kuleta
shi wa

umma.

"Ninajuaje kitakachotokea baada ya kutaja dini yangu na kabila langu? Najua hii si nchi inayofuata dini yoyote au kuendeshwa kwa misingi ya ukabila," alisema mhadhiri huyo.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Udasa), Dk Avit Mushi alisema suala hilo halikueleweka kwa sababu linaenda moja kwa moja kwenye utekelezaji, ingawa wamekuwa wakilihusisha na uhakiki unaoendelea chuoni hapo.

"Tumekuwa tukifanya uhakiki wa mara kwa mara, kwa hiyo hatukufikiria sana, lakini kilichoshtua ni huo mfumo mpya waliouleta. Nilianza kupigiwa simu kutoka kwa watu wengi wakilalamikia suala hilo," alisema.

Alisema watumishi wa chuo hicho walishtushwa na mfumo huo kwa kuwa tayari taarifa zao zipo kwa Msajili wa Hazina.

"Kimsingi hatujui sababu za ulazima wa suala hili. Hatujaambiwa sababu zaidi ya kutakiwa kujaza, kuchapisha na ku-scan kisha kuwapa wakuu wa idara ili warejeshe kwa Msajili. Hatujui lengo ni nini hasa," alisema.

Akizungumzia suala hilo, Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano katika Ofisi ya Msajili wa Hazina, Eric Mkuki, aliliambia gazeti la The Citizen kuwa ofisi inatekeleza wajibu wake kama ilivyo katika taasisi nyingine za Serikali.

Alisema Serikali kama mwajiri ina haki ya kupata taarifa za watumishi wake na kwamba Msajili wa Hazina alihusishwa kwa kuwa yeye ndiye msimamizi wa taasisi na mashirika ya Serikali hivyo anatakiwa kuwafahamu kwa kina watumishi alionao.

"Hakuna kilichokosewa katika kazi hii. Kwa hiyo nawashauri wanaohusika wajaze taarifa hizo kwa kuwa ni jambo la kawaida," alisema Mkuki.

# Mabaharia wa uvuvi wafundwa uzalendo

**Mwandishi Wetu**, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz




**Dar es Salaam.** Zikiwa zimebaki siku chache kabla msimu wa uvuvi wa kambamiti haujaanza mwaka huu, Serikali imewataka mabaharia kutanguliza utaifa mbele kwa kuzilinda rasilimali za bahari kwa manufaa ya Watanzania wote.

Msimu huu ambao ni wa tatu tangu Serikali iruhusu uvuvi wa meli kubwa baada ya kuzisitisha kwa miaka saba tangu mwaka 2010 utaanza Machi mosi na utadumu mpaka Agosti 31.

Ofisa Uvuvi Mwandamizi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Didas Mtambalika amesema Serikali imeweka mikakati kadhaa ya kuzilinda rasilimali za bahari lakini ushiriki wa wananchi unahitajika kubaini udanganyifu wowote.

"Kulikuwa na sababu kadhaa zilizoisukuma Serikali kufunga uvuvi wa kambamiti, hata uliporejeshwa kuna vigezo kadhaa vimewekwa. Meli za uvuvi zimepangwa kikanda, baharia usikubali kuhamishwa kanda kwani hilo ni kosa," alisema Mtambalika.

Ofisa huyo alisema kuna kanda tatu za uvuvi ambazo ya kwanza inajumuisha maeneo ya Pangani na Bagamoyo halafu Kisiju na Kimbiji na ya mwisho ni Kilwa. Kila chombo kitakachoruhusiwa kuvua, alisema kitapewa leseni inayotakiwa kuzingatiwa.

Aliwataka mabaharia 94 wa kampuni ya Sihai Export and Import waliokuwa wanapewa mafunzo ya maandalizi ya kufunguliwa kwa msimu huo kuhakikisha chombo wanachokiendesha kinakidhi vigezo vilivyowekwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Sihai, Michael Nachipyangu alisema wanazingatia sharia kuhakikisha kampuni yake inakua ilindaniy amiaka 10 ijayo iwe inaongoza kwa kusafirisha mazao ya bahari nje ya nchi.

"Tumejipanga vyema kufungua njia ya kunufaika na fusa za bahari, kutoa ajira na kuchangia pato la Taifa," alisema Nachipyangu.

**06**

**Miezi ambayo meli za uvuvi huruhusiwa kuvua kamba kila mwaka.**

**12**

**Idadi ya meli za uvuvi zinazoruhusiwa kuvua kwa kila msimu.**

Scanned with CamScanner

## ...eza kasi ya uwajibikaji katika maeneo ya kazi

# RC Hapi atumbua watumishi watatu

Na GHATI MSAMBA, Tarime

MKUU wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi, amemwagiza Katibu Tawala Mkoa wa Mara, kuwaondoa watumishi watatu wa Halmashauri ya Tarime katika nafasi zao za utendaji kazi kisha kuwapangia majukumu mengine nje ya halmashauri hiyo.

Hapi alitoa agizo hilo juzi, wakati akizungumza na wananchi na wafanyabishara wilayani hapa alipofanya ziara ya kikazi kusikiliza kero kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika halmashauri hiyo.

Aliwataja watumishi hao ni Ofisa Biashara Mwandamizi, Mbule Makanyaga, Ofisa Ugani Daraja II, Idd Baruna na Ofisa Sheria Mwandamizi, Alex Ifunya.

"Wananchi toeni kero zanu bila kuogopa, lakini ziwe zenye ukweli ili tuweze kuboresha Halmashauri ya Wilaya ya Tarime tuweze kuwabaini watendaji wanaotucheleweshea maendeleo kwa kukwamisha jitihada zinazofanywa na Rais wetu, Samia Suluhu Hassan," alisema.

Aidha, aliagiza Polisi Kanda Maalumu ya Tarime-Rorya kumkamata Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sirari, Wankuru Mirumbe, kisha kumfungulia mashitaka kwa tuhuma za kuiba fedha za malipo ya kodi za vibanda vya wafanyabishara ambazo aliwasainisha malipo bila kutoa risiti.

Wakati huo huo, Hapi aliahidi kutoa zawadi ya sh. 500,000 kwa Kamanda wa Polisi wilaya ya kipolisi Sirari, SSP Festo Ukulele, baada ya wananchi kumsifia hadharani kuwa anafanya kazi nzuri ya kushughulikia vitendo vya uhalifu katika eneo hilo.

Akizungumzia suala la ujenzi wa barabara, aliwataka viongozi kubuni namna ya kusajili barabara kwa kutoa mapendekezo kwa kufuata utaratibu wa kisheria na kuwashirikisha wenye maeneo sio kutumia ubabe ambao hauna tija katika utendaji wa kazi.

Mkuu huyo wa mkoa alimuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo kutafuta mtu mwenye uwezo ili ashughulikie mazingira ya usafi katika mji wa Sirari.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkazi wa Sirari, Launt Nyablangeti, aliiomba serikali kuwatengenezea mazingira mazuri wafanyabiashara waweze kulipa kodi kwa utaratibu wa kisheria, badala kutumia nguvu kama ambavyo baadhi ya watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wanafanya.

"Tunaomba mfanyabiashara afahamishwe viwango halisi na halali vya ulipaji kodi ili tuweze kuacha kufanyabiashara za magendo," alieleza.

Kwa upande wake, Meneja wa TRA Mkoa wa Mara, Adam Mtoga, alikiri kuwepo kwa malalamiko hayo ambapo aliahidi kuyafanyia kazi kwa kutoa elimu zaidi kwa wananchi.

Mkuu wa Kituo cha Forodha Sirari, Robert Busumabu, alisema biashara za magendo zimepungua kwa kiwango kikubwa, huku akitoa wito kwa wananchi kushirikiana na kituo hicho kuwafichua wanaoendesha biashara za magendo, ambapo katika eneo hilo kuna vipenyo 36 vinavyotumika kupitisha bidhaa za magendo.

UHURU UK 6.

UJENZI



NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Abdallah Ulega, akikagua maendeleo ya ujenzi wa Barabara ya Sangasanga-Sotele, Kata ya Dondwe, mkoani Pwani, mwishoni mwa wiki. Watatu kulia ni Mhandisi wa Kampuni ya Ujenzi ya Eagle investment inayojenga barabara hiyo, Hilda Makelemo. (Picha na Scolastica Msewa).

# Watumishi wadakwa na mashine feki ya mapato

Na LATIFA GANZEL, Morogoro

WATUMISHI watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro pamoja na mawakala watatu wanaotumika katika shughuli za ukusanyaji mapato ya serikali, wanashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kukutwa wakiwa na mashine feki za kukusanyia mapato.

Watu hao walikamatwa wakiwa na mashine isiyotambulika katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya halmashauri, huku mashine zingine zaidi ya 10 zinaonyesha kutumika katika mfumo wa mapato lakini hazijulikani zilipo.

Akizungumza juzi katika kikao cha bajeti cha kamati ya baraza la madiwani,

**Tuhuma**

**UDANGANYIFU**

Watumishi watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na mawakala watatu wanaotumika katika shughuli za ukusanyaji mapato wanashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kukutwa wakiwa na mashine feki za kukusanyia mapato.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa Alhaji Majid Mwanga, aliwataka watumishi wa halmashauri kuacha tabia za kutengeneza mitandao ya wizi wa fedha za serikali.

Aliwaonya kwamba Serikali ya Awamu ya Sita haitoshindwa kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria kwa wal... watakaobainika kuhujumu mapato y... halmashauri.

Akizungumzia sakata hi... Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashau... Wilaya ya Kilosa, Kisena Mabub... alisema zipo mashine 10 ambazo ba... zinaonekana kutumika kwenye mfun... lakini hazijulikani zilipo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti ... Halmashauri ya Kilosa, Wilfred Sum... alisema tayari hatua za kinidhar... zimechukuliwa kwa watumishi h... akiwemo Ofisa Tehama, Said Gwadu...

Alisema hatua zilizochukuliwa pamoja na kuwasimamisha kazi kupisha uchunguzi na hatua zingine kisheria zikiendelea kuchukuliwa ... wahusika.

Scanned with CamScanner